Journal of Literature, Languages and Linguistics
ISSN 2422-8435 An International Peer-reviewed Journal
Vol.16, 2015 

# Evaluation of Contextual Teaching of Kiswahili Proverbs in Secondary Schools in Kenya

Oduori T. Wamubi Prof. Simala, K. Inyani Profesa Mshiriki
Masinde Muliro University of Science and Technology

Prof. Ipara, I. Odeo
Kibabii University College

**Abstract**
The purpose of this research was to evaluate the contextual teaching of Kiswahili proverbs in secondary schools in Kenya. Despite the Kenya Institute of Curriculum Development (K.I.C.D) recommending in the revised syllabus that Kiswahili teachers place teaching content in real life context and environment (K.I.E. 2002), many teachers displayed inadequate knowledge on its implementation. This came to the researcher's attention through complaints registered by many Kiswahili teachers in workshops and seminars organized by the K.I.E. to sensitize teachers on how to implement the revised K.I.E. (2002) syllabus. The research objectives were: to find out whether teachers of Kiswahili teach Kiswahili proverbs contextually, to determine whether teachers have been prepared adequately to teach contextually. The research focused on Gem Sub-county, Siaya County in Kenya. The study sample comprised 14 teachers from 14 secondary schools out of 46 secondary schools in this Sub-county at the time of research. The research was guided by Contextual Teaching and Learning Theory founded by John Dewey as expounded by Vienna (2012). Contextual Teaching and Learning is a concept of teaching and learning that helps teachers relate subject matter content to real world situations (Berns and Erickson 2001). It motivates students to make connections between knowledge and its applications to their lives as family members, citizens, and workers and engage in the hard work that learning requires. This was a descriptive research. Interview, questionnaire, observation and literature review methods were used in collecting data. The data was presented in form of descriptions, tables, graphs, charts and percentages. The findings of the study revealed that though teachers used the CTL approach in teaching Kiswahili proverbs, they did not understand its principles hence did not implement it properly. Their training in the CTL approach was not exhaustive and the Kiswahili seminars and workshops organized in the field did not focus on it. Most teachers preferred the few available materials to creating their own relating these proverbs to learners' real life situations and experiences. The study will serve as a reference point for the teacher trainers to put more input in training Kiswahili teachers to implement CTL effectively. The Ministry of Education will find the research resourceful in organizing for in service, workshops and seminars aimed at addressing the challenges experienced in the implementation of CTL thereby improving Kiswahili teachers' performance. The study therefore recommends that: teacher trainers consider imparting fully the principles of the CTL to trainees in order to enable them to implement it as expected; the Ministry of Education and other stakeholders organize many seminars and workshops which should focus on this approach; prepare teaching and learning aids and publish more and adequate reference materials in this area, and advise KNEC to make a question on proverbs compulsory in national examinations in order to make teachers give its teaching the weight that it deserves. The findings of this study will be crucial in helping the educational stakeholders to find ways of improving the CTL approach as recommended in the K.I.E. (2002) syllabus.

**2.0 Ikisiri**
Utafiti huu uliazimia kutathmini ufundishaji wa methali za Kiswahili kwa kutumia mbinu ya kimuktadha katika shule za upili nchini Kenya. Mtafiti aliamua kufanya utafiti huu baada ya kubainika kuwa, licha ya Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala Nchini Kenya (Kenya Institute of Curriculum Development-K.I.C.D.) kupendekeza mafundisho kutolewa katika muktadha na mazingira halisi (K.I.E. 2002), walimu wengi walidhihirisha ukosefu wa maarifa faafu ya kutekeleza pendekezo hili. Mtafiti alitambua haya kutokana na malalamishi ya walimu mbalimbali waliohudhuria warsha na makongamano tofauti tofauti yaliyoandaliwa na taasisi hiyo ili kuwahamasisha jinsi ya kutekeleza silabasi mpya (K.I.E. 2002). Utafiti ulilenga kuchunguza ikiwa walimu walitekeleza mbinu ya kimuktadha katika kufundisha methali za Kiswahili. Madhumuni mahususi yalikuwa: kubainisha iwapo walimu wa Kiswahili walikuwa wameandaliwa kikamilifu kufundisha kimuktadha. Eneo la utafiti lilikuwa Kaunti Ndogo ya Gem, Kaunti ya Siaya nchini Kenya. Watafitiwa walikuwa walimu wa Kiswahili katika shule za upili za eneo hili. Walimu 14 walihusishwa katika utafiti huo kutoka katika shule 14 kati ya shule 46 zilizokuwa katika eneo hili wakati wa utafiti. Nadharia ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kimuktadha (UUK) ambayo iliasisiwa na John Dewey (1859-1952) ilitumiwa kuongoza utafiti huu jinsi inavyoelezwa na Vienna (2012). UUK ni dhana ya ufundishaji na ujifunzaji inayowasaidia walimu kuhusisha mafunzo na hali halisi za jamii na kuwapa wanafunzi ari ya kutoa uhusiano kati ya maarifa na matumizi yake

katika maisha yao kama wanajamii, raia na wafanyakazi (Berns na Erickson 2001). Utafiti ulikuwa wa kiuelezi. Mtafiti alitumia uchanganuzi wa matini, mahojiano, hojaji, uchunzaji na utaratibu wa usaili kukusanya data. Data hizo ziliwasilishwa kwa kutumia maelezo, majedwali, grafu, chati na viwango vya kiasilimia. Iligunduliwa kuwa ingawa walimu walifundisha methali kimuktadha, hawakuifahamu misingi yake kwa hivyo hawakuitekeleza mbinu hii kikamilifu. Maandalizi yao chuoni kuhusu mwelekeo huu yalikuwa ya kijumla na semina nyanjani zilikosa kuhusisha mbinu hii. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa na umuhimu mwingi, miongoni mwake ikiwa ni: kutumiwa na walimu na waandishi wa vitabu vya kufundishia kama marejeleo na kichocheo cha kubuni na kuandika mifano zaidi. Utafiti ulipendekeza kwamba vyuo vya kuwaandaa walimu vizingatie ukamilifu wa misingi ya UUK ili walimu wapate ujuzi kamili kuutekeleza kikamilifu, Wizara ya Elimu na washikadau wengine waandae semina na warsha nyingi zinazohusisha UUK, vifaa vinavyosheheni umk kama kanda za video viundwe pamoja na kuandika marejeleo zaidi na mitihani ya kitaifa ihusishe methali kuwa swali la lazima ili kuwafanya walimu wazingatie mada hii kwa kina na uzito unaostahili.

## 3.0 Utangulizi

Methali ni kipengele muhimu katika elimu ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Methali hufundishwa katika matumizi ya lugha, insha, fasihi simulizi na fasihi andishi. Isitoshe, methali huchangia pakubwa kutimiza madhumuni ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili nchini ambayo ni pamoja na: kwanza, kumwezesha mwanafunzi kutumia Kiswahili katika mawasiliano na shughuli za kila siku; pili, kutambua, kudadisi na kustawisha aina na tanzu mbalimbali za lugha na fasihi kwa kutumia Kiswahili; tatu, kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kuthamini fani mbalimbali za tamaduni kwa kutumia Kiswahili (K.I.E. 2002: 30).

K.I.E. (2002:28) iliwashauri walimu wa Kiswahili kufunza stadi za kusikiliza na kuzungumza kwenye muktadha na mazingira yanayoakisi hali halisi. Hata hivyo, ufundishaji mwingi wa methali, ambazo zimeorodheshwa chini ya stadi hizo, haujaonyesha umakinifu mkuu katika kuutekeleza ushauri huu. Mtagusano wa mtafiti na walimu wenzake ulidhihirisha malalamiko yao kuhusu kupungukiwa na maarifa ya kuutekeleza ufundishaji huu. Kwa vile mbinu hii ilionekana kuwa mpya, mtafiti aliona kwamba ingeambatana na changamoto fulani walimu wanapoutekeleza. Kadhalika, waandishi wa vitabu hawajajumuisha mifano ya kimaksudi ya ufundishaji wa methali kimuktadha katika maandishi yao. Isitoshe, uelekezi wa silabasi ya K.I.E. (2002) ni wa kijumla mno na usiomtosheleza mwalimu kuhusu namna ya kufundisha methali kimuktadha. Ni kutokana na hali hizi ambapo utafiti ulidhamiria kutathmini ufundishaji wa methali za Kiswahili kimuktadha katika shule za upili nchini Kenya.

Utafiti huu ulisimikwa katika misingi kama vile: kwanza, kufikia wakati huu, hakuna uchunguzi uliowahi kufanywa kubainisha iwapo walimu wa Kiswahili katika shule za upili hufundisha methali za Kiswahili kimuktadha. Utafiti wa Achillah (2010) ulibainisha kuwa walimu walitumia mbinu nyingine kufundisha msamiati tofauti na mbinu ya kimuktadha iliyopendekezwa na K.I.E. Iwapo hii ndiyo hali iliyodhihirika nyanjani kuhusu ufundishaji wa msamiati, mtafiti alipata shauku ya kuchunguza hali ilivyo katika ufundishaji wa methali kimuktadha. Msingi wa pili ni kuwa, haijadhihirishwa ikiwa walimu wa Kiswahili wameandaliwa kikamilifu kufundisha kimuktadha jinsi inavyoshauri silabasi mpya ya somo hili (K.I.E. 2002). Hii ilitokana na hali kwamba baada ya mapitio ya silabasi ya K.I.E. (2002) na mwalimu kuelekezwa kufundisha mada nyingi kimuktadha, utafiti uliofanywa ili kuchunguza utekelezaji wake si mwingi. Achillah (2010) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya 'Mbinu ya Kimuktadha katika Kufundisha Msamiati'.Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa walimu hawakuitumia mbinu hii ipasavyo. Hali hii katika ufundishaji wa msamiati ilimfanya mtafiti kutaka kuchunguza hali ilivyo katika ufundishaji wa methali za Kiswahili.

## 4.0 Madhumuni ya utafiti

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kutathmini ufundishaji wa methali za Kiswahili kwa kutumia mbinu ya kimuktadha katika shule za upili nchini Kenya. Hali hii ilitimizwa kupitia kwa madhumuni mahususi yaliyokuwa:

i. Kuchunguza iwapo walimu wa Kiswahili katika shule za upili hufundisha dhima za methali za Kiswahili kimuktadha;
ii. Kubainisha ikiwa walimu wa Kiswahili wameandaliwa kikamilifu kufundisha kimuktadha;

## 5.0 Nadharia ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kimuktadha (UUK)

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kimuktadha (UUK) iliyoasisiwa na John Dewey (1859-1952). Mwongozo wa Vienna (2012) katika nadharia hii ndio ulioegemewa zaidi katika kuelekeza utafiti huu. Kwa mujibu wa Vienna (2012), UUK ni mwelekeo katika mfanyiko wa ujifunzaji ambao husisitiza ushiriki kamilifu wa mwanafunzi ili kutafuta mafunzo yanayofundishwa na kuyahusisha na hali za maisha ambazo huhimiza wanafunzi kuweza kuyatumia mafunzo hayo katika maisha yao. John Dewey, akinukuliwa na Freeman (1999) alisema kuwa maarifa na ujuzi ambao mtu binafsi amejifunza huwa wenzo wa kuelewa na kushughulikia hali inayofuatia baadaye kwa njia mwafaka. Kwa hivyo, UUK inasisitiza umuhimu wa mazingira halisi yaliyopo, ushiriki kamilifu wa mwanafunzi, miktadha ya hali halisi za maisha, ya kibinafsi, kijamii na

kitamaduni, na tajiriba na miitiko ya ndani ya mtu katika ufundishaji na ujifunzaji. Mwanafunzi anastahili kufasili mafunzo mapya anayopewa kwa kurejelea yale maarifa ambayo tayari anayo na kuyafasili kimuktadha akiyahusisha na miktadha na mazingira halisi kwa njia inayomfaidi kuielewa jamii yake barabara.

Misingi ya nadharia hii ya UUK ni saba jinsi ilivyoainishwa na Vienna (2012). Misingi hii ni pamoja na: msingi wa ujenzi, msingi wa upekuzi, msingi wa usaili, msingi wa ujifunzaji wa kijumuia, msingi wa ufundishaji wa kifani, msingi wa kuwazia maarifa na msingi wa tathmini halisi.

Kwanza, msingi wa ujenzi au ubunizi unahusu kujenga au kukuza maarifa mapya katika akili za wanafunzi kwa kuzingatia tajiriba au uzoefu wao (Vienna 2012). Msingi huu wa uhamishaji au ujenzi hujikita katika utoaji wa maarifa mapya kutokana na maarifa ambayo mwanafunzi tayari anayajua. Katika darasa, msingi huu wa ujenzi hutekelezwa kwa kuchochea maarifa, kuyapata, kuyaelewa, kuyatumia na hatimaye kuyawazia maarifa hayo (Wijarwadi 2008:28).

Pili, kuna msingi wa upekuzi. Katika msingi wa upekuzi, ujifunzaji hujikita katika utafutaji na ugunduzi wa maarifa ambao hufanywa kwa mfanyiko wa kufikiria kwa utaratibu maalum (Vienna 2012). Maarifa hutokana na matokeo ya mfanyiko wa ugunduzi bali si ukumbukaji wa matukio mbalimbali. Mwalimu anaweza kuwahimiza wanafunzi kubainisha suala la utafiti, kuunda madhumuni ya utafiti na kuunda nadharia tete hatimaye kuenda nyanjani kukusanya data kwa uchunzaji.

Msingi wa tatu ni usaili. Katika msingi wa usaili, ujifunzaji huhusisha kuuliza na kujibu maswali (Vienna 2012). Kuuliza huakisi upekuzi au udadisi wa kila mtu binafsi nako kujibu maswali huakisi uwezo wa mtu wa kufikiria. Kuuliza maswali husaidia mwalimu kuwaongoza na kuwaelekeza wanafunzi kutambua mambo yaliyofunzwa. Lubis na Saragih (2014) wanasema kuwa usaili haufanywi tu na mwalimu bali pia hutokea miongoni mwa wanafunzi wenyewe. kuchunguza namna ambavyo walimu walishirikisha wanafunzi katika UMK ili kuufanikisha ufundishaji wa methali za Kiswahili.

Ujifunzaji wa kijumuia ni msingi wa nne. Katika UUK, matumizi ya msingi wa ujifunzaji wa kijumuia hufanywa kwa kutumia vikundi vya ujifunzaji (Vienna 2012). Wanafunzi hugawanywa katika vikundi kutegemea mseto wa uwezo wao na kasi yao ya kujifunza, vipaji vyao pamoja na shauku zao (Vienna 2012). Kila mhusika katika kikundi anafaa ahusishwe katika kujifunza huku wale wenye kasi ya juu wakihimizwa kuwasaidia wale wa kasi ya chini; nao wenye uwezo mahususi wakihimizwa kupitisha maarifa yao kwa wengine wasio na uwezo kama huo.

Tano, kuna msingi wa ufundishaji kifani. Kulingana na Vienna (2012), msingi wa ufundishaji kifani unahusu kufundisha kwa kutumia mifano ya mambo ambayo kila mwanafunzi anaweza kuiga. Hivyo basi, ufundishaji humhitaji mwalimu kuwa muigwa kwa kuonyesha mifano na mtindo wa kufuatwa na wanafunzi. Kadhalika, anafaa kuwapa wanafunzi uhuru wa kuongozana katika kutoa mifano katika shughuli za somo. Wanafunzi walio na welewa wa kiwango cha juu wanaweza kupewa nafasi ya kuwaelekeza wenzao.

Msingi wa sita ni wa kuwazia. Kwa mujibu wa Vienna (2012), msingi wa kuwazia unahusu hali ya kubwia mafunzo kwa kuyarejelea, kuyawazia upya na kuyapanga tena maarifa yaliyopatwa katika mfanyiko wa ujifunzaji.

Mwisho, kuna msingi wa tathmini halisi.Kwa mujibu wa Vienna (2012) msingi wa tathmini halisi unahusisha ukusanyaji wa data inayohusu maendeleo ya wanafunzi katika ujifunzaji. Tathmini husaidia kubainisha iwapo mwanafunzi amejifunza au la, na ikiwa tukio la ujifunzaji lina athari chanya kwenye ukuaji wake kiakili (Vienna 2012). Tathmini halisi hutumika kuelezea aina ya tathmini inayoweza kueleza matokeo ya mwanafunzi ya ari ya kujifunza, upataji wa mafunzo, na mielekeo yao kuhusu ujifunzaji mwafaka kwa shughuli za darasani (O' Malley na Pierre 1996:4).

## 6.0 Mbinu za ufundishaji shuleni

Mbinu za ufundishaji ni njia ambazo humwezesha mwalimu kutekeleza malengo ya masomo yake (Simiyu 2001). Kuna mbinu nyingi za kufundishia (Nsubuga 2000). **A**chillah (2010) anasema kwamba mwalimu hutumia mbinu itakayoafikiana na mahitaji maalum ya wanafunzi wake pamoja na mahitaji ya mtalaa. Miongoni mwa mbinu hizi ni pamoja na: usaili, mhadhara, kujadiliana, utafiti, maelezo, makundi, kutafakari, utoaji mifano na mbinu ya muktadha miongoni mwa mbinu nyingine. Wingi wa mbinu za kufundishia unasababisha ugumu wa kujadili mbinu zote zilizopo (**A**chillah 2010). Kwa mintarafu hii, utafiti ulijikita katika kufafanua kwa kina mbinu ya kimuktadha ambayo ndiyo nguzo kuu katika kazi hii.

## 6.1 Mbinu ya kimuktadhaMM

Mbinu ya kimuktadha ni mojawapo ya mbinu za kufundisha. Ijapokuwa kuna mbinu nyingi za kufundisha, mbinu hii ya MM ndiyo kiini cha utafiti huu.

### 6.1.2 Maana

Ufundishaji wa kimuktadha ni mfumo wa ufundishaji ambao humruhusu mwanafunzi kujitambulia maana katika somo halafu alihusishe somo hilo na hali ya maisha katika mazingira yake (Kamaruddin na Amin, 2009). Ili kutimiza haya, inamlazimu mwalimu wa methali kufundisha wanafunzi kwa kuwafanya waelewe miktadha ya

matumizi yake. Hili linasisitizwa na Hymes (1974) anaposema kwamba ili kuongea lugha kwa ufasaha, ni lazima ujue msamiati wake pamoja na muktadha sahihi wa matumizi. Hili ni dhihirisho kuwa mbinu ya kimuktadha ni muhimu katika kutekeleza wazo hili. Katika ufundishaji kwa mbinu hii, mwalimu hutarajiwa tkuzingatia utiaji wa methali katika miktadha mwafaka ya matumizi hasa muktadha wa hali halisi za maisha ya jamii.

Kulingana na Mieder (2004), methali hutegemea muktadha na hufasiriwa katika muktadha zinamotokea. Muktadha huu unaweza kuwa wa mazingiza asili ama kitovu cha methali kutokana na msamiati uliotumiwa au muktadha wa kimatumizi. Kwa mfano, kulingana na K.L.B. (2011), methali zinaonyesha miktadha mbalimbali:

*42. Mwacha mila ni mtumwa.*

Methali hii inarejelea muktadha zalishi wa kijamii na muktadha wa kimatumizi wa utamaduni ambapo watu wanahimizwa kuuzingatia bila kuupuuza. Kwa kufuata mbinu hii, methali huwekwa pamoja iwapo zimezalishwa katika miktadha sawa ama ikiwa zinaweza kutumiwa katika miktadha au mazingira yanayofanana.

Ufundishaji wa methali kwa mbinu hii ya muktadha unafafanuliwa zaidi na Budden (2010). Akirejelea ufundishaji wa methali na misemo katika Kiingereza kama lugha ya pili, Budden (2010) anaeleza kuwa kabla ya mwalimu kuanza kufundisha methali, afikirie iwapo wanafunzi wake wako tayari kujifunza mada hiyo ya methali. Pia ajiulize ikiwa wanafunzi wana uwezo wa kujitolea mifano ya methali zao wenyewe. Hatimaye, mwalimu apange kipindi chake kwa njia ya kuvutia wanafunzi na kutimiza kikamilifu somo hilo lake kwa namna ya kumridhisha.

Kwanza, mwalimu azifundishe methali zinapotokea katika miktadha ya maisha ya wanafunzi kama vile: katika kusoma na kusikiliza au zinapojitokeza katika mazungumzo ya mwalimu mwenyewe. Pili, mwalimu azitie methali katika vikundi kulingana na mada kisha azifungamanishe na shughuli zingine za mada mfano wa zile methali zinazohusu sehemu za mwili au kilimo. Hii hurahisisha uwezo wa wanafunzi kuzielewa na kuzikumbuka.Tatu, mwalimu atumie michoro ili kudumisha ukumbukaj kwa mfano, anaweza kutumia mchoro wa zabuni moja mkononi na mbili kichakani (Budden 2010). Mchoro kama huo utawarahisishia wanafunzi kukumbuka methali husika;

43. *Heri moja mkononi kuliko kumi nenda uje tena*.

Nne, mwalimu atumie shughuli za kukutanisha, kama vile wanafunzi kupewa kadi zenye vipande nusunusu vya methali ili watafute, kuchagua na kuoanisha vipande vingine vya kuzikamilisha.Tano, mwalimu awaulize wanafunzi iwapo methali husika zimo katika lugha yao ya kwanza.Sita, mwalimu azitie methali hizo katika muktadha unaofaa kisha achague baadhi ya wanafunzi waigize muktadha huo ili kusisitiza maana.

Budden (2010) anamshauri mwalimu kuwa asiwarundikie wanafunzi methali nyingi katika kipindi kimoja; afadhali awafundishe methali tano tano katika kila kipindi.

**6.1.3 Aina za miktadha**

Kwa mujibu waWarriner na Francis (1977), kuna aina mbili kuu za miktadha. Aina hizo ni: muktadha wa kiisimu na muktadha wa hali halisi

**6.1.3.1 Muktadha wa kiisimu**

Kulingana na Warriner na Francis (1977), muktadha wa kiisimu huhusisha utumiaji wa matini au sentensi ambazo zinajumuisha msamiati unaodhamiria kukisia maana lengwa (Achillah 2010). Kwa hivyo, ikiwa ni ufundishaji wa methali katika muktadha huu, maana yake itakisiwa kupitia kwa sentensi au matini ambamo methali husika imetumiwa. Yule (2004) anasema kwamba muktadha wa kiisimu hudokeza maana za maneno katika muktadha wa maneno mengine. Hii inadhihirisha kwamba methali nazo zinaweza kufundishwa kwa muktadha wa kiisimu kwa kukisia maana na matumizi yake katika muktadha wa maneno katika mazingira ya methali husika katika matini fulani.

**6.1.3.2 Muktadha wa hali halisi**

Muktadha wa hali halisi hurejelea mazingira ambamo neno linatumiwa (Achillah 2010).Hii ina maana kuwa, muktadha wa hali halisi utahusisha mazingira ambamo methali inatumika. Achillah (2010) anasema kwamba ni lazima kushuhudia vitu au matendo katika hali halisi ili kung'amua maana ya vitu na matendo hayo. Kwa hivyo, ni muhimu kushuhudia matukio yanayohusu methali fulani kama msingi wa kuifundisha kwa mbinu ya muktadha ili kuielewa ipasavyo kwa mfano, katika shughuli za mazishi, kilimo, usafiri, vita, sherehe, uzazi, malezi, kuchumbiana, dini miongoni mwa shughuli nyingine za jamii. Utafiti huu ulichunguza namna ambavyo walimu walihusisha matukio katika mazingira halisi kama msingi wa kufundisha methali kwa mbinu ya kimuktadha.

**6.1.4 Misingi ya mbinu ya muktadha**

Misingi ya mbinu hii ya ufundishaji na ujifunzaji wa muktadha ni saba. Misingi hii ni: msingi wa ujenzi, msingi wa upekuzi, msingi wa usaili, msingi wa ujifunzaji wa kijumuia, msingi wa ufundishaji wa kifani, msingi wa kuwazia na msingi wa tathmini halisi (Vienna 2012).

**6.1.4.1 Msingi wa ujenzi**

Kwa mujibu wa Vienna (2012), msingi wa ujenzi unahusu kujenga au kukuza maarifa mapya katika akili za wanafunzi kwa kuzingatia tajiriba au uzoefu wao. Msingi huu ambao pia huitwa uhamishaji au ujenzi hujikita katika utoaji wa maarifa mapya kutokana na maarifa ambayo mwanafunzi tayari anayajua. Katika darasa, msingi

huu wa ujenzi hutekelezwa kwa kuchochea maarifa, kuyapata, kuyaelewa, kuyatumia na hatimaye kuyawazia maarifa hayo (Wijarwadi 2008:28).

Kwa mujibu wa msingi wa ujenzi, mwalimu alitarajiwa kuanza kipindi cha methali kwa kuwauliza wanafunzi kutambua methali wanazozifahamu kwanza. Baadaye, mwalimu anatarajiwa kutaja methali zingine ama zenye maana sawa au maana kinyume kisha aendeleze hatua zingine za somo. Utafiti huu ulichunguza iwapo walimu walizingatia mahitaji ya msingi huu katika kufundisha methali kwa MM.

**6.1.4.2 Msingi wa upekuzi**

Kulingana na Vienna (2012), msingi wa upekuzi hukita ufundishaji katika udadisi na ugunduzi unaofanywa kwa kufikiria kwa utaratibu maalum. Utaratibu huu huhusisha kuchagua mada, kuunda madhumuni ya utafiti kisha nadharia tete na baadaye kuenda nyanjani kuzipima kwa utafiti. Suala la kimsingi katika upekuzi ni wanafunzi kujitafutia wenyewe habari na ujuzi (DNE 2003:12).

Kwa mujibu wa msingi wa upekuzi, mwalimu anatarajiwa kuwahusisha wanafunzi katika kuunda madhumuni na nadharia tete kuhusu mada ya methali hatimaye wakaenda pamoja nyanjani kwenye jamii zao kuzitafitia methali, ama kwa kuzikusanya au kujifunza methali hizo katika muktadha halisi wa chimbuko ama muktadha wa kimatumizi.

**6.1.4.3Msingi wa usaili**

Katika msingi wa usaili, ujifunzaji huhusisha kuuliza na kujibu maswali (Vienna 2012). Kwa hivyo, mfanyiko wa ufundishaji na ujifunzaji huongozwa kwa shughuli za kuulizana maswali kuhusu mada pamoja na kuyajibu maswali husika. Kwa mujibu wa Lubis na Saragih (2014), usaili hufanywa na mwalimu na hata hutokea miongoni mwa wanafunzi wenyewe. Usaili mwafaka husaidia: kutambua uwezo wa wanafunzi kuelewa somo, kuhimiza wanafunzi kujifunza, kuchochea udadisi wa wanafunzi kuhusu masuala fulani, kuelekeza wanafunzi kwenye matamanio yao na kuongoza wanafunzi katika kutafuta chochote au kufikia mahitimisho ya jambo lolote (Vienna 2012).

Msingi huu unamtarajia mwalimu kufundisha methali kwa kushirikisha wanafunzi katika usaili. Mwalimu anafaa kuwauliza wanafunzi maswali ya kuwaelekeza huku akiwaruhusu kumuuliza pamoja na kuulizana miongoni mwao. Pia wanafunzi wapewe nafasi ya kujibu maswali katika kila hatua ya mafunzo ya methali.

Msingi huu ulitumiwa katika kuchunguza namna ambavyo walimu walitumia msingi wa usaili katika vipindi vya methali. Walimu walichunguzwa kama walihusisha wanafunzi katika usaili pamoja na jinsi walivyosambaza usaili huo katika kipindi kizima.

**6.1.4.4Msingi wa ujifunzaji wa kijumuia**

Msingi wa ujifunzaji wa kijumuia hutekelezwa kwa kutumia vikundi vya ujifunzaji (Vienna 2012). Wanafunzi hugawanywa kwenye vikundi vya wanafunzi wenye sifa ainati kutegemea uwezo na kasi yao ya kujifunza, vipaji vyao na shauku zao. Kila mhusika katika kikundi anafaa ahusishwe katika kujifunza huku wenye kasi ya juu wakihimizwa kuwasaidia wale wa kasi ya chini; nao wenye uwezo mahususi wakihimizwa kuwapitisha maarifa kwa wengine wasio na uwezo kama huo. Muundo huu wa kushirikisha ni namna ya kujifunza kwa kubadilishana mawazo, kuitikia na kuwasiliana na wanafunzi wengine (CORD1999). Kwa hivyo, mwalimu hushauriwa kuhimiza wanafunzi kukuza mbinu za kushirikiana kwenye mafunzo.

Kulingana na msingi huu, mwalimu anastahili kufundisha methali kwa kugawa wanafunzi katika vikundi vya kujadiliana mada hii. Inafaa vikundi hivi viundwe kutegemea mambo mbalimbali kama vile: uwezo na kasi ya wanafunzi ya kujifunza, vipaji vyao na shauku zao.

Utafiti huu ulitumia msingi wa ujifunzaji kijumuia kutathmini matumizi ya vikundi katika ufundishaji wa methali,vigezo vilivyotumiwa na walimu kuunda vikundi hivyo, namna walivyotumia vikundi hivyo wakati wa somo na jinsi wanafunzi walivyohusishwa katika vikundi hivyo.

**6.1.4.5Msingi wa ufundishaji wa kifani**

Msingi wa ufundishaji wa kifani unahusu ufundishaji wa kutumia mifano ya mambo ambayo kila mwanafunzi anaweza kuiga. Msingi huu unadhihirisha kwamba mwalimu anapaswa kuwa muigwa wa mafunzo anapoonyesha mtindo wa kufuatwa na wanafunzi. Kadhalika, anafaa kuwapa wanafunzi uhuru wa kuongozana katika kutoa mifano katika shughuli za somo. Wanafunzi walio na welewa wa kiwango cha juu wanaweza kupewa nafasi ya kuwaelekeza wenzao.

Kwa mujibu wa msingi huu, mwalimu anahitajika kufundisha methali kwa kuwaonyesha wanafunzi mfano wa kuigwa. Pia mwalimu anastahili kuwapa wanafunzi nafasi ya kuongoza wenzao katika somo la methali.Msingi huu unamtarajia mwalimu kuhusisha ufundishaji kifani katika kila hatua ya kipindi kizima.

Msingi huu ulitumiwa na utafiti katika kubainisha matumizi ya wanafunzi kuwaongoza na kuwaelekeza wenzao katika kuzichambua methali wakifuata mwongozo wa walimu waliohusishwa katika utafiti huu.

**6.1.4.6Msingi wa kuwazia**

Kulingana na Vienna (2012), msingi wa kuwazia unahusu hali ya kurejelea kuwazia maarifa yaliyopatwa katika mfanyiko wa ujifunzaji. Baada ya kiasi fulani cha mafundisho, mwanafunzi anafaa kupewa wakati wa kufikiria tena kwa makini yale aliyofundishwa ili kumfanya ayakumbuke, kuyaelewa na kuyabwia katika akili yake.

Msingi huu unamtarajia mwalimu wa somo la methali kwa MM kuwapa wanafunzi nafasi ya kuwazia mafunzo ili kuzielewa na kuzibwia methali hizo akilini mwao. Pia mwalimu anastahili kusambaza nafasi za wanafunzi kuziwazia methali katika kipindi kizima tangu mwanzo hadi mwisho.Utafiti ulitumia msingi huu kuchunguza namna ambavyo walimu walifundisha methali kwa kuzingatia vigezo vya msingi huu.

**6.1.4.7Msingi wa tathmini halisi**

Msingi wa tathmini halisi unahusisha ukusanyaji wa data inayohusu maendeleo ya wanafunzi katika ujifunzaji (Vienna 2012). Tathmini husaidia kubainisha iwapo mwanafunzi amejifunza au hajajifunza, na ikiwa tukio la ujifunzaji lina athari chanya kwenye ukuaji wake kiakili. Welewa wa wanafunzi hutathminiwa kwa kuchunguza utendaji wao au jinsi wanavyowasilisha mawazo yao, kazi zao za ziada, tamrini, ripoti, vitendo vyao wakati wa somo na majaribio ya kuandikwa (DNE 2003:19). Tathmini halisi hutumika kuelezea aina ya tathmini inayoweza kueleza matokeo ya mwanafunzi ya ari ya kujifunza, upataji wa mafunzo, na mielekeo yao kuhusu ujifunzaji mwafaka kwa shughuli za darasani (O' Malley 1996:4).

Kwa mujibu wa msingi wa tathmini halisi, mwalimu anahitajika kutumia tathmini kubainisha ujifunzaji wa wanafunzi. Tathmini halisi inafaa kusambazwa katika kipindi chote tangu mwanzo hadi mwisho.Utafiti ulitumia vigezo vya msingi huu kuchunguza namna ambavyo walimu walitumia tathmini katika somo la methali ili kubaini welewa wa wanafunzi.

## 7.0 Ufundishaji wa dhima za methali kimuktadha

Mwalimu anatarajiwa kufundisha dhima za methali kimuktadha. Kipengele hiki cha dhima za methali ni mojawapo ya vipengele vikuu vinavyozingatiwa katika ufundishaji wa methali. Dhima asilia ya methali ni dhima ya kufundisha kwa vile husheheni busara, ukweli, maadili na mitazamo ya kitamaduni (Malinauskiene 2004; Mieder 2004:3; Abadi 2000; Obelkevich 1994). Methali zinaweza kushauri, kufariji, kuhimiza, kutoa maoni na kusisimua matumaini, kutamauka na unyenyekevu (Nippold nw. 2001a:2). Kwa mujibu wa Mieder (1993), hakuna mwisho wa matumizi ya methali. Hii inamaanisha kwamba methali haziwezi kutenganishwa na shughuli za maisha katika jamii yoyote ile.

Wakati wa utafiti, walimu walitarajiwa kutaja vipengele wanavyofundisha katika methali. Walimu wote 14 (100%) waliandika kwamba dhima za methali ni kipengele kinachopewa uzingativu mkubwa sana na walimu katika ufundishaji wao. Jambo hili lilidhihirishwa kwa mifano mingi ya dhima za methali ambazo walimu walisema kwamba wao huzifundisha. Njia za mahojiano na uchunzaji zilionyesha kwamba walimu walitumia misingi ya mbinu ya kimuktadha kufundisha dhima za methali. Misingi hiyo ni kama vile: msingi wa ujenzi, usaili, ujifunzaji wa kijumuia, ufundishaji kifani, kuwazia na tathmini halisi. Hata hivyo, hakuna mwalimu aliyetumia misingi hiyo yote katika kipindi kimoja. Dhima za methali zilizofundishwa ni pamoja na:

### 7.1 Methali kama burudani

Walimu wote 14 (100%) walieleza kwamba wao hufundisha wanafunzi dhima ya methali kuwa burudani. Burudani katika methali hutokana na usanii pamoja na ufasaha wa mpangilio wa maneno yanayozijenga ambayo huvutia akili ya wanajamii na kuwafanya wazifurahie. Walimu wote 14 (100%) walitumia mtazamo wa kiutamaduni kuhusisha methali zenye burudani na jamii, na baadhi yao walitumia msingi wa UUK wa usaili kupata mchango wa wanafunzi kama ilivyo mifano ifuatayo:

*155. Mwana mtamba kule hushinda mzee wa kale.*

*156. Mzika pembe ndiye mzua pembe.*

Kwa msingi wa ufundishaji kifani, walimu walidhihirisha kwamba waliwaeleza wanafunzi burudani katika methali ya 155 kutokana na takriri ya silabi {-le} na {m-}. Hata hivyo, walimu hao hawakuelewa msingi huu ipasavyo na hata hawakujua kuwepo kwa msingi huu bali mtafiti alijitambulia kutokana na maelezo yao.

### 7.2 Methali na maadili ya jamii

Methali hizi zinabeba maadili yanayotarajiwa kuzingatiwa katika jamii.Hudhamiria kukuza jamii yenye matendo mema.Mafunzo yanayobebwa ndani ya methali huzifanya ziwe nyenzo za kufunza maadili (Yankah 2001). Kutokana na maadili haya yaliyomo, wanafunzi wa shule za upili wanaweza kuadilika, nao wakayapitisha kwa wanajamii wengine wa kizazi cha sasa wanaotangamana nao katika jamii pamoja na vizazi vingine vya baadaye.

Walimu walipohojiwa, walimu 3 (21%) walitaja kwamba walitumia methali za aina hii mara nyingi kuwaadilisha wanafunzi ndani ya vipindi vya Kiswahili hata nje ya vipindi hivi, walimu 7 (50%) wakatumia kiwastani huku walimu 4 (29%) wakitumia mara chache. Hali hii inaoana na mwelekeo wa kiutamaduni ambapo walimu hao walibuni miktadha darasani. Mifano iliyopatikana kutoka kwa walimu ni:

*157. Heshima si utumwa. (heshima)*

Heshima miongoni mwa wanajamii huweza kuhimizwa kwa kutumia methali hii. Watanasihiwa kwamba wanapomheshimu mtu, si ishara ya kudhihirisha unyonge wala si hali ya kutawaliwa bali ni desturi ya utu.

*158. Ada ya mja hunena muungwana ni vitendo.*

Methali hii inasheheni maadili ya uungwana ambapo watu wanahitajika kuuonyesha kupitia kwa matendo mema

ila si kwa mavazi na maneno matupu.
*163. Mchama ago hanyele huenda akauya papo.*
Tunapohama mahali si vizuri kuwakosea wenyeji heshima kwani huenda kukatokea haja ya kutulazimisha kurudi mahali pale kuwataka usaidizi.
*164. Ukipewa shubiri usichukue pima.*
Ni vyema mtu kutosheka na kile akipatacho hata kama ni kidogo.
Walimu 12 (86%) walisema kuwa mifano hii ilitajwa na wanafunzi katika vikundi vyao vya ujifunzaji kijumuia na ufundishaji kifani ambayo ni misingi ya MM. Kwa hivyo, walimu 12 (86%) walifundisha kwa mbinu ya kimuktadha. Utafiti ulibainisha kuwa walimu walitumia misingi hii kwa tukizi bila kufahamu inavyostahili kutumiwa. Walimu hao hawakufanya maandalizi ya kimaksudi ya kutumia misingi hii ya UUK kwa vile hawakuijua.

**7.3 Methali kama falsafa ya maisha**
Uchanganuzi wa matini ulidhihirisha kuwa kuna methali zinazotambulisha jinsi jamii inavyoelewa, kuamini na kuyachukulia mambo fulani yanayotendeka katika jamii yao. Kwa hivyo, methali huonyesha mambo yanayopendwa na yale yasiyopendwa na wanajamii husika. Mahojiano baina ya mtafiti na walimu katika utafiti huu yalibainisha kuwa dhima hii huzingatiwa na walimu wanapofundisha methali. Kupitia kwa mifano waliyotoa, ilidhihirika kwamba walimu walifundisha kwa mbinu ya muktadha kwa namna tofauti tofauti. Kwa mfano, walimu 6 (43%) walisema kwamba walifundisha kwa mwelekeo wa kufundisha methali katika uandishi wa insha. Walimu hao walieleza kuwa katika vipindi vya insha za methali, walitumia mtazamo wa kisaikolojia kueleza vipengele vya kiisimu methali hizi kama muundo, maana ya maneno yaliyozijenga halafu wakaisheheneza katika muktadha wa utamaduni wa jamii. Walimu hawa walifafanua mifano ifuatayo:
*165. Ucha Mungu si kilemba cheupe.*
Methali hii inaonyesha falsafa ya jamii inayochukia na kukashifu unafiki. Wanafiki hawapendwi katika jamii kama hii.
*166. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.*
Methali hii nayo inaonyeha falsafa ya jamii inayopenda bidii na kujitafutia riziki.
Kupitia njia ya uchunzaji darasani, mtafiti aligundua walimu 8 (57%) walitumia misingi ya usaili, ufundishaji kifani na kuwazia. Waliwashirikisha wanafunzi kutoa mifano mbalimbali. Katika mojawapo ya vipindi, wanafunzi walitoa mfano huu:

**7.4 Methali na urathi wa utamaduni**
Kwa mujibu wa Hanzen (2010), methali ni sehemu ya kila lugha na hata kila utamaduni. Hivi ndivyo methali zinavyochukuliwa kama nyenzo za kutambulisha na hurithisha utamaduni wa jamii (Matei 2011). Kutokana na hali hii, wanajamii hasa wanafunzi nchini Kenya wanapojifunza methali hizi za Kiswahili ambazo ni zao la jamii, hujifunza utamaduni wa jamii ya Wakenya ilivyo kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa. Hali hii huelekea kuchangia utimizaji wa madhumuni ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili (K.I.E. 2002). Wakati wa mahojiano, utafiti uligundua kwamba walimu 10 (71%) walidhihirisha kuwa walitumia msingi wa ujenzi, usaili na ufundishaji kifani kufundisha mifano ifuatayo:
*168. Mwosha husitiri maiti.*
Ni desturi ya wanajamii za kiafrika kuosha maiti kabla ya kuizika.Yule anayeosha maiti hastahili kutangazia watu wengine hali ya maiti husika. Vivyo hivyo, watu wanashauriwa wasitangaze udhaifu wa wenzao.
*169. Mwana kidonda, mjukuu kovu.*
Methali hii inaakisi utamaduni wa mtu kumshughulikia mtu wake wa ukoo kwanza kabla ya kumrejelea rafiki.

**7.5 Methali na upambaji lugha**
Methali ni kiungo muhimu katika upambaji wa lugha. Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na walimu, utafiti ulitambua kwamba japo walimu walitambua umuhimu wa methali katika kupamba lugha, ni wachache sana waliohimiza wanafunzi kuzitumia katika mawasiliano nje ya kipindi cha Kiswahili. Walimu wote 14 (100%) walisema kwamba wanafunzi walikumbana na methali nyingi za kupamba lugha katika miktadha ya fasihi, vifungu vya ufahamu na uandishi wa insha. Hii ilidhihirisha kwamba walimu hao walifundisha methali katika muktadha wa matini ya fasihi, ufahamu na uandishi wa insha. Kwa kufanya hivyo, walitumia mwelekeo mseto.

**7.6 Methali na Maonyo**
Methali za Kiswahili husheheni maonyo kwa wanajamii dhidi ya mambo fulani. Methali kama hizi hulenga kuwatahadharisha wanajamii kuhusu hatari fulani au jambo lolote lisilopendeza ama lisilokubaliwa na jamii yao. Wakati wa mahojiano, mtafiti alifahamishwa na walimu wote 14 (100%) kuwa wao huzingatia na kufunza dhima hii. Mifano ifuatayo ya methali ambazo zinadhihirisha hali hii ndizo ambazo zilijitokeza nyanjani wakati wa mahojiano:

*173. Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.*
Methali hii inaonya waja dhidi ya kuwadharau au kuwakosea heshima watu waliowasaidia kwani huenda wakawa na haja ya kuwataka msaada tena.
*174. Ibilisi wa mtu ni mtu.*
Watu wajihadhari na wenzao kwani maafa mengi yampatayo binadamu husababishwa na mtu mwenzake kutokana na chuki na uadui wao. Wasiwe wa kujilaumu au kulaumu Mungu kabla ya kuwachunguza wenzao.
*176. Kikulacho ki nguoni mwako.*
Mtu anayekudhuru ni yule wa karibu nawe kwa sababu anazifahamu siri zako kwa undani.
*177. Mchimba kisima huingia mwenyewe.*
Watu wanaowafanyia wenzake mabaya huenda mbaya hayo yakawafika pia na kuwahasiri wao wenyewe.
*178. Enga kabla ya kutenda.*
Chukua tahadhari kabla ya kufanya jambo fulani.
*179. Siku za mwizi ni arobaine.*
Mwizi anapoiba hutokea siku anayoweza kupatikana.
*182. Mkataa chinjo hupata mtanda.*
Methali hii inamwonya mtu anayekataa kitu kidogo kizuri kwa kutaka kikubwa huenda akaishia kupatwa na mazito ya kuangamiza.

### 7.7 Methali na Ushauri wa Jamii

Busara inayoshehenezwa katika methali huchukuliwa kama kielekezi cha mienendo ya wanajamii. Wanajamii wanapokumbana na methali za jinsi hii, wao huweza kupata uelekezi mwafaka wa kuwafanya watambue namna ya kukabiliana na changamoto za maisha huku wakidumisha uhusiano mwema unaozingatia maadili ya jamii husika.
Hojaji zilizojazwa na walimu zilionyesha kuwa walimu wote 14 (100%) walifundisha dhima hii ya methali katika muktadha wa matini za fasihi, ufahamu, ufupisho, na insha. Utafiti huu uliweza kutambua kwamba walimu wote 14 (100%) walizifafanua methali hasa zile zilizotumika katika miktadha ya fasihi, ufahamu, ufupisho na insha jinsi ambavyo zilitumiwa kutoa ushauri kwa wanajamii wakiwemo wanafunzi. Kwa mfano:
*183. Kufanya kosa si kosa, kosa ni kurudia kosa.*
Kupitia kwa methali hii, waja wananasihiwa kuepuka kutenda makosa tena na tena. Kadhalika, wasiache mambo yaharibike bila kuyasuluhisha kwa kuogopa kutenda kosa fulani kwani watu daima si wakamilifu.
*184. Mpanda ngazi hushuka.*
Watu wenye madaraka ama waliofanikiwa katika jamii wasiwadharau na kuwasumbua wanyonge na wasiojiweza kwani huenda wakaharibikiwa na hali yao nzuri.
*185. Ngozi ivute ili maji.*
Ni heri waja wasisitesite jambo linapoanza kuharibika bali walirekebishe mapema kabla halijaharibika kabisa.
*187. Mwana akinyea kinyeo hakikatwi.*
Methali hii inawaaidhi wazazi au wanajamii kuwa wasamehevu kwa wakosaji kwa vile si vizuri kuwashikia kinyongo.
*189. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.*
Anayekataa ushauri mwema anaopewa na wazazi au wakuu huishia kuharibikiwa na mambo.
Katika kufundisha dhima hii, mahojiano na walimu yalibainisha kwamba walimu 9 (64%) walishirikisha wanafunzi kutoa mifano na kuongoza wenzao huku walimu 5 (36%) wakitawala kipindi chote kwa kutumia ufundishaji kifani ulioegemea mwalimu kwa kutoa mifano ambayo iliigwa na kuandikwa na wanafunzi.

### 7.8 Methali na tafkira

Methali hutumiwa kuwafikirisha wanajamii. Wanajamii wanapopata methali fulani, wao hulazimika kufikiria kwa kina ili kuihusisha maana fiche ya methali hiyo wanayoifahamu na ule muktadha unaorejelewa. Methali hizi zinapokuwa ngeni kwao, wao hujifikirisha ili kupata fasili yake kulingana na muktadha wa matumizi. Njia hii huwalazimisha kupanua mawazo yao na kuyakomaza zaidi.
Utafiti uligundua kupitia kwa uchunzaji kuwa walimu 6 (43%) walitumia misingi ya mbinu ya muktadha ambayo ilikuwa: msingi wa usaili, msingi wa kuwazia na msingi wa tathmini halisi. Baadhi ya methali za aina hii kama zilivyojitokeza katika ufundishaji wa watafitiwa ni:
*191. Kila mchuma janga hula na wa kwao.*
Kwa kusikia methali hii, wanafunzi walilazimika kutafakari kwa makini ili waelewe ukweli wa busara iliyo ndani kwamba mtu anayetafuta shida huwahasiri watu wake.
*192. Nyani haoni kundule.*
Methali hii iliwafanya wanafunzi watafakari ndipo wakaelewa kuwa nyani kukosa kuona kundule inabeba busara ya mja kuona tu matatizo ya wengine bila kujua kwamba yeye ana matatizo kama hayo.

**7.9 Methali na mshikamano wa jamii**

Methali huwa wenzo mwafaka wa kuwafanya wanajamii kuwa na sauti moja katika shughuli zao za kila siku hususan iwapo methali husika ni zile ambazo zinaendeleza uhusiano mwema baina ya watu wakati wanapozitumia. Watu huzitumia jinsi hii kusuluhisha migogoro yao na kuisahau kwa manufaa ya jamii nzima. Mahojiano baina ya mtafiti na watafitiwa yalibainisha kwamba walimu wote 14 (100%) walidhukuru dhima hii katika harakati zao za UMK. Walitumia msingi wa ujenzi ambapo waliwahitaji wanafunzi kuwatajia mifano ya methali za kuhimiza mshikamano wa kijamii. Baada ya wanafunzi kutaja mifano yao, walimu walitoa mifano yao na wakaijadili na wanafunzi. Miongoni mwa mifano iliyotajwa ni pamoja na:

*193. Mtu pweke ni uvundo.*
*194. Mtu ni watu.*
*195. Kidole kimoja hakivunji chawa.*

Methali zote zilizotajwa hapo juu hutumiwa kwa lengo la kudumisha umoja miongoni mwa wanajamii. Huwasaidia wanajamii kuleta udugu bila kuwabagua wengine.

*196. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.*

Rafiki atakutoroka wakati wa shida hata ingawa mlishirikiana kufurahia maisha. Hata hivyo, mtu wa ukoo atajitolea mhanga kukusaidia kutatua shida yako.

*197. Ndugu chungu jirani mkungu.*

Ndugu kwa ndugu wana uhusiano wa dhati zaidi kuliko mtu na jirani au marafiki. Kwa hivyo ni heri tusiamini na kuwathamini majirani zaidi kuliko ndugu.

**7.10 Methali kama himizo**

Katika kutenda shughuli mbalimbali, baadhi ya wanajamii huweza kufikia hatua ya kutamauka. Hali hii huzua haja ya kuwapa moyo ili waendelee kushughulika ipasavyo hadi wapate matokeo mema. Methali zenye kuwapa watu hao moyo hufaa wakati kama huu. Mahojiano ya mtafiti na walimu yalidhihirisha kuzingatiwa na wote 14 (100%) kwa methali zenye kuhimiza katika UMK kwa mtazamo wa kiutamaduni ambapo methali zilifafanuliwa kwa mujibu maisha ya jamii za wanafunzi. Mfano ambao mwalimu mmoja alibainisha ni:

*200. Mui huwa mwema.*

Mtenda maovu wakati mwingine hubadilika na kuanza kutenda mema. Kwa hivyo wanafunzi walihimizwa kuwa wasichoke na waovu bali wazidi kuwashauri mwishowe huenda wakabadilika.

**7.11 Methali na faraja**

Watu wanapopatwa na simanzi au mambo mazito maishani, wanaweza kuliwazwa ama kutulizwa kwa methali za aina hii. Alipowahoji walimu, mtafiti alitajiwa mifano ifuatayo ambayo inasheheni ujumbe wa kuliwaza:

*201. Baada ya dhiki faraja.*

Mwalimu mmoja alitumia methali hii kuwashauri wanafunzi kwamba wakati wa shida wazitafutie utatuzi kwa uvumilivu. Huenda shida hizo zikaisha na hatimaye raha ikafuata.

*202. Hakuna bahari iso mawimbi.*

Wanafunzi walielezwa kuwa kila hali ina magumu yanayoambatana nayo. Kwa hivyo, ni afadhali kuivumilia hali ngumu inayowakumba bila kuhangaika huku na kule wakijisononesha. Mtafiti alifahamishwa na walimu wengi 11 (79%) kuwa walishughulikia dhima hii katika miktadha ya riwaya, hadithi fupi, ushairi na ufahamu. Ni walimu wachache 3 (21%) waliofundisha methali hizi katika miktadha ya hali halisi. Hawa walizitumia kuwatuliza wanafunzi wakati wa majonzi, misiba au mikasa.

**7.12 Methali na Sifa**

Kuna Baadhi ya methali ambazo hudhamiriwa kusifu au kubeba maudhui ya kusifu. Mahojiano ya walimu yalibainisha kwamba walimu wachache 3 (21% ) walizitumia methali zenye maudhui haya kuhimiza tabia njema miongoni mwa wanafunzi wao nje ya darasa la Kiswahili jinsi wanavyotarajiwa na ufundishaji wa kimuktadha. Walimu wengine 11 (79%) walifundisha darasani kwamsingi wa ufundishaji wa kifani kwa kuzichambua methali na kuzihusisha na maisha halisi. Hali hii ilidhihirisha msingi wa ujenzi katika UUK. Mifano ya methali za sifa zilizotolewa ni pamoja na:

*203. Jina jema hung'aa gizani.*

Wanafunzi walielezwa kwa methali hii kwamba uzuri wa mtu hutambulika tu popote hata bila kujitangaza. Walimu hao 11 (79%) waliwatajia wanafunzi mifano ya watu shuleni na nchini wanaostahiki kuheshimiwa kwa uzuri wao hata bila kujitapa.

*204. Chema chajiuza, kibaya chajitembeza.*

Walimu walitumia mfano huu kusisitizia wanafunzi umuhimu wa kuwa na sifa njema kwani ukiwa hivyo utatafutwa kinyume cha mwenye sifa mbovu ambaye atajisumbua kwa kujitangaza ili ajulikane. Walimu 4 (29%) kati ya walimu 14 (100%) walishirikisha wanafunzi kutaja mifano ya watu wanaoweza kurejelewa na methali hii katika jamii ya darasa na shuleni mwao.

*205. Mnyonyore haunuki, hupendeza mauaye.*
Walimu waliotoa mfano huu walieleza wanafunzi wao kwamba mtu mwenye sifa nzuri anaweza kuishi katika mazingira ya watu waovu naye akatokea kuwa mwadilifu bila kuiga maovu ya waovu hao.

**8.0 Maandalizi ya walimu kufundisha kwa mbinu ya muktadha**
Nunan (1997) anapozungumzia ufundishaji wa sarufi ya Kiingereza, anasema kwamba walimu wanastahili kusaidia wanafunzi kuona kuwa mawasiliano mwafaka yanahusisha uwiano kati ya ufasili wa kiuamilifu na ukubalifu rasmi. Hii hutokea kwa kuwapa kazi zinazoiga uhusiano baina ya vipengele vya kisarufi na muktadha wa mazungumzo ambamo vinatokea (Halliday 1985). Kwa jinsi hii, methali pia, kama ilivyo sarufi huweza kueleweka barabara iwapo walimu watawasaidia wanafunzi kuzitia katika muktadha wake wa matumizi. Hali hii inawezekana kama maandlizi mwafaka yamefanyiwa walimu hao.

Wakati wa mahojiano, mtafiti aliwauliza walimu ikiwa waliandaliwa kufundisha kwa mbinu ya kimuktadha. Kati ya walimu 14 (100%), walimu 8 (57%) waliofuzu walikubali kuwa waliandaliwa chuoni.Walimu 5 (36%) waliofuzu hawakukumbuka iwapo walipata maandalizi hayo. Mwalimu 1 (7%) ambaye alikuwa hajafuzu alisema kwamba hakuandaliwa kufundisha kwa muktadha. Hata hivyo, wale walimu wanane waliokiri kuandaliwa chuoni walisema kwamba maandalizi yalikuwa ya kijumla katika mada mbalimbali bali hazikuwa mahususi kwa ufundishaji wa methali. Hali hii ilidhihirisha upungufu ambapo walimu wengine walijitafutia maarifa hayo wenyewe vitabuni ambavyo pia ni haba jinsi ilivyobainishwa na walimu 5 (36%) ambao hawakukumbuka kama waliandaliwa chuoni. Hali kama hii inazua tatizo ambalo huenda likatatiza utekelezaji wa matakwa ya silabasi ya ufundishaji kwa mbinu ya kimuktadha. Data ya maandalizi ya walimu imeonyeshwa katika jedwali la 1:

| Maandalizi | Idadi ya walimu | Asilimia |
|---|---|---|
| Walioandaliwa chuoni | 8 | 57 |
| Wasiokumbuka | 5 | 36 |
| Wasioandaliwa | 1 | 7 |
| Jumla | 14 | 100 |

**Jedwali la 3: Maandalizi ya walimu kufundisha kimuktadha**

**9.0 Ufundishaji wa methali kwa kutumia mbinu ya kimuktadha kijumla**
Ufundishaji wa kimuktadha unahusisha hali ya mafunzo kutiwa katika miktadha mahususi ya maisha ya wanajamii. Mtafiti alidhamiria kuchunguza iwapo walimu wa Kiswahili walikuwa wakitekeleza ushauri wa silabasi ya K.I.E (2002) wa kutia mafunzo kwenye muktadha.

Walimu walipoulizwa kama walikuwa wakiutumia mbinu hii ya kimuktatha kufundisha methali, majibu yao kwenye hojaji yalionyesha kwamba walimu 13 (93%) walikubali kuwa waliitumia ilihali mmoja alikataa. Mwalimu huyo alisema kwamba wanafunzi hujifanyia utafiti kuhusu mada ya methali chini ya tanzu fupi za fasihi simulizi. Hata hivyo, alipoeleza wakati wa mahojiano kwamba yeye alieleza methali kwenye matini ya riwaya, tamthiliya na hadithi fupi, mtafiti alimjumuisha kwenye orodha ya walimu walioitumia MM. Kwa hivyo, walimu wote 14 (100%) walifundisha methali kimuktadha. Hili ni dhihirisho kwamba mbinu ya kimuktadha inatumiwa na walimu kufundisha methali za Kiswahili. Hata hivyo, iwapo walimu wanatumia mbinu hii kwa kuzingatia mahitaji yake yote ni suala ambalo lilihitaji ufafanuzi zaidi katika sehemu zinazofuata katika sura hii.

**9.1 Matumizi mahususi wa misingi ya mbinu ya muktadha**
Vienna (2012) aliainisha misingi saba ya nadharia ya UUK. Misingi hii ni: kwanza, msingi wa ujenzi, pili, upekuzi, tatu, usaili, nne, ujifunzaji wa kijumuia, tano, ufundishaji wa kifani, sita, wa kuwazia na saba, ule wa tathmini halisi.

Walimu walipoulizwa iwapo walitumia misingi saba ya UUK wakati walipokuwa wakifundisha methali kimuktadha, wote walikiri kwamba hawakuifahamu misingi hii ya ufundishaji na ujifunzaji wa kimuktadha (UUK). Hata hivyo, baada ya mtafiti kuwafafanulia, walionyesha kuwa walitumia baadhi ya misingi hiyo ingawa hawakujua inavyoitwa. Hii ilikuwa ishara kwamba kulikuwa na walakini katika maandalizi yao ya matumizi ya mbinu hii. Hali hii imefafanuliwa zaidi jinsi ifuatavyo:

**9.1.1 Msingi wa ujenzi**
Rachmadiarti (2002) anasema kwamba katika msingi huu, wanafunzi hujenga hali mpya kutokana na maarifa yao ya awali. Pia ujifunzaji hushehenezwa katika kujenga bali siyo kupokea maarifa. Walimu wote 14 (100%) walikubali kuutumia msingi huu. Walijenga au kukuza maarifa mapya katika akili za wanafunzi kwa kuzingatia tajiriba ama uzoefu wao. Walisema kuwa walianza vipindi vyao kwa kuwapa wanafunzi nafasi ya kutaja methali walizofahamu, ndipo wakajenga hapo kwa kuongeza ama methali zenye maana sawa nazo au zenye maana kinzani, kisha wakaendelea kufundisha vitengo vingine vya methali hizo. Hata hivyo, walimu hao hawakujua msingi huu kwa jina lake bali mtafiti alijitambulia tu kutokana na maelezo yao katika mahojiano na utendaji wao darasani wakati wa uchunzaji.

**9.1.2 Msingi wa upekuzi**

Katika msingi huu, ujifunzaji hujikita katika udadisi na ugunduzi unaofanywa kwa kufikiria kwa utaratibu maalum. Maarifa hayatokani na idadi ya matukio ya kukumbukwa bali hutokana na matokeo ya mfanyiko wa ugunduzi. Huu ni mfanyiko wa uchunzaji unaozalisha uelewaji na wanafunzi hujifunza kutumia mbinu za kufikiria kwa hali ya juu (Rachmadiarti 2002). Mintarafu hii, walimu wanapojiandaa wanastahili kuunda mafunzo yanayowaruhusu wanafunzi kujitambulia mambo kwa kuwashirikisha katika kubainisha suala la kuchunguzwa, kuunda madhumuni, nadharia tete na kuenda nyanjani kuzipima kwa utafiti kwa kukusanya data na kuzifanyia maamuzi.

Katika ufundishaji wa methali, ni walimu 8 (57%) pekee waliokubali kuwa waliutumia msingi huu huku 6 (43%) wakisema kwamba hawakuutumia. Hata hivyo, walimu waliokubali kuwa wao huutumia waliutumia kihafifu kwani hawakufuata mtindo wa kufanya maandalizi maalum na kuenda kufanya utafiti nyanjani pamoja na wanafunzi. Badala yake, wote 8 (57%) waliwatuma tu wanafunzi kutafuta methali za jamii zao, kisha wakazitafsiri au kuzitafutia zile za Kiswahili zenye ujumbe unaokaribiana nazo. Walimu hawa wote hawakuenda nyanjani pamoja na wanafunzi kutafitia methali.

**9.1.3 Msingi wa usaili**

Katika msingi huu, ujifunzaji huhusisha kuuliza na kujibu maswali. Kuuliza hutazamiwa kuakisi upekuzi ama udadisi wa kila mtu binafsi, nako kujibu maswali huakisi uwezo wa mtu kufikiria. Kuuliza husaidia mwalimu kuwaongoza na kuwaelekeza wanafunzi kutambua mambo yaliyofunzwa. Usaili faafu husaidia: kwanza, kutambua uwezo wa wanafunzi kuelewa somo, pili, kuhimiza wanafunzi kujifunza, tatu, kuchochea udadisi wa wanafunzi kuhusu kitu fulani, nne, kuelekeza wanafunzi kwenye matamanio yao, na kuongoza wanafunzi katika kutafuta chochote au kufikia mahitimisho ya kitu chochote (Vienna 2012). Kwa mujibu wa Dewey (1970), mazingira mwafaka katika elimu ni yale yanayowachochea wanafunzi kuuliza na kutafuta kujibu maswali. Hivyo basi ni muhimu kwa walimu kujenga mazingira yanayomfanya mwanafunzi ajihisi huru kushiriki katika mafunzo ya mada ya methali kwa MM kwa kuuliza maswali na hata kujibu mengine. Maswali haya yanaweza kuulizwa wanafunzi wenzake na mwalimu pia. Japo kwenye miitiko yao katika hojaji walimu wote 14 (100%) walikiri kuutumia msingi huu, udadisi zaidi wakati wa mahojiano ulidhihirisha matumizi finyu yasiyozingatia vipengele vyake vyote jinsi vinavyojitokeza hapo juu. Walimu wengine walitumia masaili kuchochea michango ya wanafunzi katika tamrini, mijadala na mazungumzo ya kawaida darasani. Hata hivyo, maswali yaliyotumiwa katika sehemu ya kati ya kipindi yalikuwa machache kwani walimu wote 14 (100%) waliuliza asilimia kubwa ya maswali mwanzoni na mwishoni mwa kipindi. Hii ilionyesha kuwa matumizi ya msingi huu yanahitaji kupigwa msasa.

**9.1.4 Msingi wa ujifunzaji wa kijumuia**

Kwa mujibu wa Rachmadiarti (2002), msingi huu huhusisha kikundi cha watu wenye shughuli ya kujifunza ambapo kushirikiana na wengine, kubadilishana maarifa na mawazo huhimizwa. Wanafunzi hugawanywa kwenye vikundi vya wanafunzi wenye sifa ainati kutegemea uwezo wao na kasi yao ya kujifunza hata vipaji na shauku zao (Vienna 2012). Kila mhusika katika kikundi anafaa ahusishwe katika kujifunza huku wenye kasi ya juu wakihimizwa kuwasaidia wale wa kasi ya chini nao wenye uwezo mahususi wakihimizwa kuwapitishia wengine wasio na uwezo kama huo (Vienna 2012). Walimu 10 (71%) walikiri kuutumia msingi huu huku 4 (29%) wakikosa kuutumia.

Mtafiti alipowasaili zaidi wakati wamahojiano, walimu 10 (71%) walioutumia msingi huu walitumia vikundi vya wanafunzi vilivyotumiwa katika masomo mengine yote katika silabasi yao ya shule za upili. Hivi vilikuwa vikundi ambavyo viliundwa kwa kuzingatia uwezo wao wa kiakademia peke yake bali havikuundwa kwa kutilia maanani sifa zingine za wanafunzi kama vile kasi yao, vipaji vingine visivyo vya kiakademia, na shauku zao jinsi inavyotakikana katika msingi wa ujifunzaji wa kijumuia. Walimu hawa walitoa sababu ya kukosa nafasi ya kufanya hivyo kutokana na majukumu mengi waliyo nayo shuleni kando na ufundishaji wa Kiswahili. Huu ni udhaifu ambao utafiti uliona kwamba utafutiwe suluhisho.

**9.1.5 Msingi wa ufundishaji wa kifani**

Ni mfanyiko unaozingatia utoaji wa mifano ambayo wengine huipima na kuishughulikia na kuichunguza (Rachmadiarti 2002) kwa mfano, namna ya kutumia kifaa, au kutamka vifungu vya lugha ya kigeni au mwanafunzi stadi wa kusoma shairi kutolea wengine mfano wa jinsi ya kulisoma (Vienna 2012). Hivyo basi, katika UUK, ufundishaji wa kutoa mifano una manufaa ya kuwafanya wanafunzi waepuke ujifunzaji wa makisio ya kidhahania uliohusisha ukariri sisisi wa mafunzo.

Matokeo ya mahojiano yalibainisha kwamba walimu 5 (36%) pekee waliutumia msingi huu, japo kihafifu mno, huku walimu 9 (64%) wakikosa kuutumia. Hali hii inabainisha kuwa ni walimu wachache waliotumia msingi huu. Hata wale walioutumia hawakuutumia kikamilifu, hali ambayo inahitaji kushughulikiwa.

**9.1.6 Msingi wa Kuwazia**

Msingi huu unahusu hali ya kurejelea na kuwazia maarifa yaliyopatwa katika mfanyiko wa ujifunzaji wa awali (Vienna 2012). Kwa kufanya hivi, ujifunzaji hurekodiwa kwenye utambuzi wa mwanafunzi na hivyo basi kuwafanya wawe wahusika katika maarifa hayo. Katika UUK, mwalimu huwapa wanafunzi nafasi ya kurejelea

au kukumbuka yale waliyojifunza. Mwalimu humruhusu mwanafunzi kufasili huria tajiriba yake mwenyewe ili aweze kufahamu na kufanya uamuzi kutokana na ujifunzaji huo. Walimu 6 (43%) walikubali kuutumia msingi huu wa kwa kuwaagiza wanafunzi waeleze maana, matumizi ya methali pamoja na kusimulia kisa kifupi. Hata hivyo, walionyesha matumizi yasiyo ya kina.Walitumia kwa tukizi mwanzoni na katikati ya kipindi. Walimu hao 6 (43%) waliutumia msingi huu kwa kiwango kikubwa mwishoni mwa kipindi ilihali walifaa kuutumia katika kipindi chote tangu mwanzo hadi mwisho. Ili kuimarisha mbinu ya muktadha, msingi huu unafaa kupigwa msasa.

**9.1.7 Msingi wa Tathmini Halisi**

Msingi huu unahusisha kutathmini maarifa ya wanafunzi na utendakazi wao kupitia kwa shughuli muhimu za kimuktadha (Rachmadiarti 2002). Kwa mujibu wa Vienna (2012), msingi huu unahusisha ukusanyaji wa habari/data inayohusu maendeleo ya wanafunzi katika ujifunzaji. Anaendelea kueleza kuwa tathmini husaidia kubainisha iwapo mwanafunzi amejifunza au la, na ikiwa tukio la ujifunzaji lina athari chanya kwenye ukuaji wake kiakili. Otieno (2012) anatambua kwamba mwalimu hawezi kufahamu kama wanafunzi wameelewa mambo wanayofundishwa bila kuwapa mtihani. Hata mwalimu hutumia tathmini kufahamu utendaji wake mwenyewe, ikiwa amefaulu au la (Farrant 2002).Vienna (2012) anasisitiza kwamba tathmini hii hufanywa kwa kuifungamanisha na shughuli za ujifunzaji. Tathmini hufanywa kwa njia ya kuendelea wakati ule ule wa shughuli za ujifunzaji. Matokeo ya utafiti kutokana na hojaji za walimu yalibainisha matumizi ya msingi huu kwa walimu wote 14 (100%) ili kukadiria weledi wa methali miongoni mwa wanafunzi. Mahojiano na uchunzaji ulidhihirisha kwamba walimu wengi 10 (71%) walitumia masaili, mijadala, tamrini, mazungumzo ya kawaida na kazi ya ziada huku walimu 4 (29%) wakitumia mitihani hasa ya uandishi wa insha za methali. Mwalimu mmoja miongoni mwa hao kumi aliongezea matumizi ya nyimbo za kusifu masomo. Usetaji wanjia mbalimbali za kutathmini ulidhihirika miongoni mwa walimu wengi 10 (71%).

**10.0 Hitimisho**

Uchanganuzi wa data iliyokusanywa wakati wa utafiti ulidhihirisha masuala anuwai yaliyohusiana na mada ya utafiti, 'ufundishaji wa methali za Kiswahili kwa kutumia mbinu ya kimuktadha'. Masuala haya ni kama ifuatavyo:

Kwanza, ilitambuliwa kwamba walimu waliotafitiwa walifuzu kufunza somo la Kiswahili isipokuwa mmoja aliyekuwa katika chuo kikuu. Pia walimu walikuwa na tajiriba ya kutosha kufundisha ya akali ya miaka minne. Wengi wa walimu hawa waliandaliwa kufundisha kimuktadha katika chuo kikuu. Hali hii ilitarajiwa kuakisiwa katika utendaji wao katika ufundishaji wa methali kwa mbinu ya muktadha. Hata hivyo, iligunduliwa kuwa maandalizi hayo yalikuwa finyu. Walimu walionyesha ufahamu hafifu wa mwelekeo huu wa ufundishaji wa kimuktadha.

Pili, ilibainika kwamba matarajio ya walimu hawa kufidia upungufu wa maandalizi katika mbinu hii kupitia kwa semina na warsha za Kiswahili yaligonga mwamba. Japo walimu walihudhuria semina na warsha hizi, mada zilizoshughulikiwa hazikuhusisha mbinu ya muktadha. Iligunduliwa kuwa mara nyingi waandalizi walikuwa wafanyabiashara. Ingawa Wizara ya Elimu kupitia K.I.E. iliandaa baadhi ya semina na warsha hizo, maandalizi haya yalitokea baada ya kipindi kirefu mno. Isitoshe, utafiti pia uligundua kwamba walimu wengine walikosa kuhudhuria baadhi ya semina na warsha hizo kwa kukosa ufadhili wa shule ikidhaniwa kuwa mada warsha na semina hizo ilikuwa ile ile ya semina na warsha za awali hivyo basi shule ikakosa kuona haja ya kuwafadhili kila mara. Matokeo ni walimu kujitafutia njia nyingine za kuimarisha utendakazi wao katika umk huku wengine wakitamauka.

Nne, ilifahamika kwamba walimu wote 14 (100%) walitumia mbinu hii ya kimuktadha kufundisha methali. Hata hivyo, matumizi haya yalidhihirika kuwa yasiyokamilika kwa vile walimu hawakufahamu kuwa mbinu hii ilikuwa na misingi yake maalum inayostahili kufuatwa. Waliitumia misingi hiyo kinasibu tu bila kujua inavyoitwa wala sifa zake bainifu.

**Vifupisho**

CHAKISIA.......................Chama Cha Kiswahili Cha Siaya.
C.T.L................................Contextual Teaching and Learning Approach.
K.C.S.E...............................Kenya Certificate of Secondary Examination.
K.I.C.D ..…………………Kenya Institute of Curriculum Development.
K.I.E...................................Kenya Institute of Education.
K.N.E.C..............................Kenya National Examinations Council.
Mb......................................Maana batini/maana ya ndani ya methali.
Mh .....................................Mhariri.
MM………………………..Mbinu ya Kimuktadha
nw.......................................na wengine.
UMK...................................Ufundishaji wa Methali Kimuktadha.
UUK ..................................Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kimuktadha.

**MAREJELEO**

Abadi, M. C. (2000).“Proverbs as ESL curriculum.” Proverbium 17:1-22.
Achillah, A.R. (2010). “Matumizi ya Mbinu ya Kimuktadha Katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili Katika Shule za Upili za Wilaya ya Kakamega.”
Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Masinde Muliro.
Berns, R. G.& Erickson, P. M. (2001). *Contextual teaching and learning: Preparing students for the new economy.* Columbus, OH: National Dissemination Center for Career and Technical Education.
Budden, J. (2010). *Proverbs and idioms/Teaching English*/British Council/BBC.
https://www.teachingenglish.org.uk/language.../teaching.../proverbs-Retrieved on10/4/2014
Carol P. Harrell (h.t) Department of English Kennesaw, State University: ilitolewa Tarehe 29/4/2013
Carter, R. & Long, M.N. (1991).*Teaching Literature*. New York: Longman.
Chesebe, M.(2010). K.C.S.E. Golden tips: *Stadi za Uandishi wa Insha*. Nairobi: Moran Publishers.
*Contextual Instruction*.Accessed on 22nd of July 2009.http://www.cpal.net/course/module4/m4_contextual_instruction.html
CORD, (1999).*Teaching Science Contextually: The Cornerstone of Tech Prep.* Waco, Texas 76702-1206: United States of America. February 1999.
Department of National Education.( 2003). Pendekatam Kontekstual (Contextual Teaching and Learning-CTL). Jakarta. Depdiknas.
Dewey, J. (1970). *The child and the Curriculum*.Chicago University Press.
Eliza, (2012).http://teachingrocks.ca/wp-content/uploads/2012/5/proverbs.worksheet.pdf Retrieved on 11/4/2014
Farrant, J.S. (2002). *Principles and Practices of Education*. Singapore: Longman Group. U.K.
Freeman, D. (1999). “Changing Teaching: Insight Into Individual Development In The Contexts Of School” in Christopher Ward and Willy Reynanda
(Eds.), Language Teaching: A New Insights for the Language Teacher (Singapore: SEAMEO Regional Language Center), p.34
Gathumbi, A.W. (2005). *Principles & Techniques in Language Teaching: A Text For Teacher Educators, Teachers and Pre-service Teachers.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Halliday, M.A.K. (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Arnold. Heath, S.B. 1992. ‘Literacy skills or literate.
Hymes, D. (1974). *Foundations of Sociolinguistics: An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania
K.I.E (2002).*Secondary Education Syllabus*.Vol. 1. Nairobi: K.I.E.
K.I.E. (2006).*Kiswahili Sekondari*: Mwongozo Mwalimu. Nairobi: K.I.E.
K.N.E.C . (2008). *The year 2007 K.C.S.E. Examination Report. Kenya National Examination Council.* Nairobi: Government Printers.
Kagwa, F. M. & Waihiga, G. (2007).*Kamusi Changanuzi ya Methali*.Macmillan Kenya.
Kamaruddin, N. K. Md & Amin, Z.Md (2009). Implementation Of Contextual SysteIn Mathematics Course Universiti Tun Hussein Onn Malaysia (UTHM)
K.L.B. (2011).*Kiswahili kwa Kidato cha Pili.*Toleo la 2, Nairobi, K.L.B.
Longhorn (2011).*Kamusi ya Karne ya 21.* Nairobi. Longhorn Publishers.
Ligami, P. na Barasa, S. “ Tahakiki ya Methali za Kiswahili” katika CHAKITA-Kenya na Twaweza Communications, (2006) Fasihi Simulizi. Twaweza Communications.
Lubis, P. M. & Saragih, W. (2014). The effect of using contextual teaching and Learning (CTL) method on students’ achievement in Writing recount text
Matei , K.A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi wa shule za sekondari*. Nairobi: Oxford.
Mieder, W. (1993).*Proverbs Are Never Out of Season. Popular Wisdom in the Modern Age.* New York: Oxford University Press.
Mieder, W. (2004).*Proverbs - A Handbook*.Westport, CT; Greenwood Press.
Musau, P.M. na Chacha, L.M. (2001). *Mbinu za Kisasa za Kufundisha Kiswahili*. Nairobi. K.L.B.
Mwachilumo,P. (2013). “Kuandika Insha Bora ya Methali” *Taifa Leo*, Tarehe 19/2/2013. Nairobi: Nation Media Group.
Ngure, A. (2004). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari: Maandalizi Kamili ya K.C.S.E*, Toleo jipya, Phoenix publishers, Nairobi.
Nippold, M. A. Allen, Melissa M. & Kirsch, Dixon I. (2000). “How adolescents Comprehend unfamiliar proverbs: The role of top-down and bottom-up processes.” *Journal of Speech, Language, and Hearing Research* 43:621-630.
Nippold, M.A, Allen, Melissa M. & Kirsch, D.I. (2001).*Proverb comprehension as a function of reading proficiency in preadolescents*. Language, Speech, and Hearing Services inSchools 32:90-100.
Nippold, M.A, Power, R & Taylor, C.L. (2001).*Comprehending literally- true versus literally-false proverbs.*

*Child Language Teaching & Therapy17*:1-18.

Norrick, N. R. (1985). *How Proverbs Mean: Semantic Studies in English Proverbs.* Amsterdam: Mouton. Available from:*http://books.google.com/books* [Accessed 28, April 2014]

Norrick, N. R. (1985). *How Proverbs Mean. Semantic Studies in English Proverbs.* Berlin: Mouton.

Norrick, N. R. (1994). "Proverbial perlocutions. How to do things with proverbs." In Wolfgang Mieder (Ed.), *Wise Words. Essays on the Proverb*. New York:

Nsubuga E.H.K (2000). *Fundamentals of Educational Research.* Kampala: MK Publishers (UK) Ltd. Uganda.

Nsubuga E.H.K (2000). *The Teacher as a Professional*. Kampala: MK Publishers (UK) Ltd. Uganda.

Nunan, D. (1997). *Teaching Grammar In Context. Department of Applied Linguistics.* Hong Kong University. Retrieved from internet in August, 2012.

Nunan, D. (1997). *Teaching Grammar In Context. Department of Applied Linguistics.* Hong Kong University. Retrieved from internet in August, 2012.

O' Malley, A. M. & Pierre. L. V. (1996). *Authentic Assessment for English Learners.* USA: Addison – Wesley Publishing Company.

Obelkevich, J. (1994). "Proverbs and social history." In Wolfgang Mieder (Ed.), *Wise Words.Essays on the Proverb*. New York: Garland Publishing Inc., 211-252.

Otieno, E.A (2012). "Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha-Ishara Katika Ufundishaji wa Sarufi ya Kiswahili Kwenye Shule za Msingi Mkoani Nyanza; Kenya." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Masinde Muliro. Kakamega, Kenya.

Prabhu, N.S. (1987). *Secondary Language Pedagogy: A perspective.* Oxford: Oxford University Press.

Rachmadiarti, P. (2002) *Charting Your Course: How to Prepare to Teach More Effectively*. (English ed.). Madison, WI: Atwood Publishing Using Contextual Instruction to Make Abstract Learning Concrete.http://goliath.ecnext.com/coms2/gi_0199-738644/

Simiyu, A.M. (2001). *The System Approach to Teaching.*Eldoret. Western Education Publishers.

TUKI (2006). (3rd edition) – *English – Swahili Dictionary*. TUKI Dar-es-Salaam.

TUKI (2012). (Toleo la tatu) – *Kamusi ya Kiswahili Sanifu:* Oxford, Dar-es-SAalaam.

Using Contextual Instruction to Make Abstract Learning Concrete.
http://goliath.ecnext.com/coms2/gi_0199-738644/Using-contextual- instruction

Vienna (2012).*Contextual teaching and learning.* Onlinesyariah.com2014/02/components ofctlhttp://www.learning.htmlRetieved on February, 2014.

Viungo vya Nje (Methali za Kiswahili) Ilitolewa Kwenye Mtandao Tarehe 28/2/2013
http://www.mwambao.com/methali.htm,
http://kiswahili.de/modules.php?name=SwahiliProverbs,
ttp://mwanasimba.free.fr/E_methali_01.htm,
http://www.angelfire.com/yt/chibilamsane/methali.html

Walter, J. P. (2014). Proverbs: An Introduction.http//www.redwritethink.org/classroom/ resource/lesson-plans/proverbs-introduction184.html

Wamitila K.W. (2001). *Kamusi ya Methali.*Longhorn Publishers, Nairobi.

Wamitilia K.W. (2001). *Lulu za lugha 2: Kamusi ya Methali*. Longhorn, Nairobi.

Warriner, J.E. & Francis G. (1977).*English Grammar and Compositon*. New York, Harcourt BraceJovanovich Publishers.

Waweru, M. n.w. (2009) *Dira ya Uandishi wa Insha: Mazoezi na Marudio kwa Shule za Upili.* Nairobi. K.L.B.

Wizara ya Elimu (2008).*Kiswahili kwa Kidato cha 4.* Nairobi: K.L.B.

Wizara ya Elimu, (2011).*Kiswahili kwa Kidato cha 2*. Toleo la tano, Toleo la. Nairobi. K.L.B.

Wizara ya Elimu (2009).*Kiswahili kwa Kidato cha 3*, Toleo la tatu. Nairobi: K.L.B.

Yankah, K. (2001). "Proverb." in Duranti, A. (ed.). 2001. Key Terms in Language and Culture: 201-203. Malden, MA: Blackwelland American Anthropology Association.

Yule, G. (2004) *The Study of Language*. 2nd edition. Cambridge, Cambridge University Press.